



CATHOLIC DIOCESE OF BUNGOMA



Dedication & Opening of the Christ The King Cathedral Bungoma

May 8th 2021



Prayer for the Diocese

Heavenly Father,

In calling us to follow Christ Your Son
You have made us members of this Diocese,


Which is a local Church,

Teach us to serve You faithfully in its boundaries
and to make it manifest the universal Church for us,
Help both religious and laity who form part of it
to work together in true Christian Unity.

May Your Word be truly proclaimed and heard here
and may Your sacraments, especially the Eucharist,
be faithfully administered and devoutly received.

Grant that our Diocese may provide a fervent example
Of the power of Your Word and the might of Your Salvation
For Your honour Glory and our salvation. Amen

From Peoples Prayer Book, No. 1206-



UJE, ROHO MTAKATIFU (Sekwensya)

1. Uje Roho Mtakatifu, tuangaze toka mbingu roho zetu kwa mwangao.
2. Uje Baba wa maskini, uje mtoa wa vipaji, uje, mwanga wa mioyo.
3. Ee Mfariji mwema sana, ee Rafiki mwa (a) nana, ewe raha mustarehe.
4. Kwenye kazi u pumziko, kwenye joto burudisho, u mfutaji wa machozi.
5. Ewe mwanga wenye heri, uwajaze waamini neema yako mioyoni.
6. Bila nguvu yako wewe, mwanadamu hana kitu, kwake yote yana kosa.
7. Osha machafuko yetu, panyeshee pakavu petu, na kuponya majeraha.
8. Ulegeze ukaidi, pasha moto ubaridi, nyosha upotevu wote.
9. Wape waamini wako, wenye tumaini kwako paji zako zote saba.
10. Wape tuzo ya fadhila, wape mwisho bila ila, wape heri ya milele.
11. Amina, Aleluya, Amina, Aleluya, Amina, Aleluya.



CATHOLIC DIOCESE OF BUNGOMA

**DEDICATION AND OPENING OF
CHRIST THE KING CATHEDRAL
BUNGOMA**

SATURDAY 8TH MAY 2021

BY:

**H.E. Archbishop Hubertus Matheus Maria van Megen -
Apostolic Nuncio to Kenya and South Sudan**

TABLE OF CONTENT

Rite Of Dedication Of A Church	Pg 1
Entrance	Pg 2
Part II Blessing & Sprinkling Of Water	Pg 3
Part III Liturgy Of The Word	Pg 5
Part IV Prayer Of Dedication	Pg 11
Part V Anointing Of The Altar	Pg 14
Part VI Incensation Of The Altar	Pg 16
Part VII Lighting Of The Altar	Pg 17
Part VIII Liturgy Of The Eucharist	Pg 25
Part IX Inauguration Of The Blessed Sacrament	Pg 30
Nyimbo Za Roho Mtakatifu	Pg 31

UJE ROHO MTAKATIFU

Sop: Uje Roho mtakatifu

All: Mapajio kutushushia uje roho x2

1. Utupatie hekima – Uje roho
Utupatie shauri - Uje roho
Utupatie akili - Uje roho
Utupatie na nguvu - Uje roho
Utupatie elimu - Uje roho
Utupatie ibada - Uje roho

MPOKEENI ROHO MTAKATIFU

Mpokeeni huyo roho mtakatifu mfariji pokeeni na mapaji yake saba x2

1. Yeye ni hekima atupa hekima maarifa. Yeye ni akili twayajua mema na mabaya.
2. Yeye ni elimu atuelimisha mambo yote. Yeye ni faraja atufariji kwa matatizo.
3. Yeye ni shauri twapata shauri kwake Mungu. Yeye ndiye nguvu twapata nguvu twafanya kazi.
4. Yeye ni ibada twamuabudu mwenyezi Mungu. Yeye ni uchaji roho wake atujaza nguvu.

NJOO WANGU MFARIJI (18-1t/b)

All: Njoo wangu mfariji, yako shusha mapaji

Roho Mungu njoo x1

Sop/Alto:

1. Hekima nishushie, Mungu nimfuatie
Roho Mungu Njoo
2. Akili nijalie, imani nizidie, Roho Mungu njoo x1
3. Nieneze shauri, nishike njia nzuri, Roho Mungu njoo x1
4. Nizidishie nguvu n'sifanye ulegevu, Roho.....
5. Elimu nieleze, hakika niongoze, Roho.....

TWAKUOMBA UJE ROHO MFARIJI

1. **Sop:** Twakuomba uje roho mfariji

All: Uje roho mtakatifu mfariji

Sop: Twakuomba uje kutufariji

All: Uje roho mtakatifu mfariji

Nyoyo zetu ni latari yako uzipambe kwa mapaji yako uje roho mtakatifu mfariji x2

2. Wewe ndiwe mleta kwetu mapaji, uje roho mtakatifu mfariji, wewe ndiwe Baba mwema na mpaji, uje roho mtakatifu mfariji.
3. Tunakuomba uwezo na akili, uje roho mtakatifu mfariji, tunaomba mapendo ya kweli, uje roho mtakatifu mfariji.

NJOO ROHO MTAKATIFU TOKA MBINGU

Sop- All

**Njoo Roho- Mtakatifu toka mbingu
Jaza neema ndani ya viumbe x2**

1. Tn. Tunaomba akili tufahamu vizuri
All. Jaza neema ndani ya viumbe x1
2. Tusaidie kwa shauri, tuchague vizuriJaza...
3. Nguvu iwe tayari, tushindane hodari, jaza...
4. Utujaze elimu mafundisho tuelewe...Jaza
5. Tuwashie ibada na uchaji wa Mungu, Jaza.....

NJOO ROHO MTAKATIFU TOKA MBINGU

Njoo Roho mtakatifu, shusha yako mapaji ili niwe imara x2

(karibu nakukaribisha, moyoni mwangu Shusha yako mapaji niwe imara)x2

1. Sop. Roho wa hekima Roho wa shauri, Roho wa ibada Njoo moyoni mwangu.
2. Roho wa elimu Roho wa akili, Roho mfariji wa uchaji Njoo moyoni mwangu.
3. Roho wa imara unitie nguvu, Roho mfariji Njoo unifariji.

POPE FRANCIS



H.E. Archbishop Hubertus Matheus Maria van Megen
Apostolic Nuncio to Kenya and South Sudan



Bishop Joseph Obanyi Sagwe
Bishop of Kakamega, Kenya. Apostolic Administrator of Bungoma.




Rev. Fr. Christopher Wanyonyi Paul
Parish Priest



BUNGOMA DIOCESE-ADMINISTRATIVE BOUNDARIES

KEY

1. Ndal
2. Naitiri
3. Tongaren
4. Maliki
5. Webuye East
6. Misikhu
7. Kibuk
8. Kaptateleo
9. Chelelemuk
10. Kocholia
11. Cheptais
12. Kimilili
13. Sirisia
14. Chebukaka
15. Sikusi
16. Bukembe
17. Kimatuni
18. Kimwanga
19. Myanga
20. Kanduyi



21. Bungoma
22. Samoya
23. Kibabii
24. Kongoli
25. Amukura
26. Chakol
27. Kisoko
28. Butula
29. Butunyi
30. Bumutiru
31. Bumala
32. Buhuyi
33. Busia
34. Bulanda
35. Lwanya
36. Mundika
37. Nangina
38. Dahiyo
39. Port Victoria
40. Sirimba
41. Magombe

NYIMBO ZA ROHO MTAKATIFU

MOYO WANGU WAMTUKUZA

Uje, Roho Mtakatifu, uju mfariji x2

- | | |
|----------------------------------------------------------------|-----------------------------------------------------|
| 1. Uje, Baba wa maskini – uje, mfariji
Roho mtoa wa vipaji- | 6. Ulegeze ukaidi –
Pasha moto ubaridi – |
| 2. U rafiki mwema sana –
U mfutaji ;wa machozi – | 7. Bila zako wewe –
Mwanadamu hana kitu – |
| 3. Uwe mwanga wa mioyo
Uangaze toka mbingu – | 8. Kwenye kazi u pumziko
Kwenye joto burudisho – |
| 4. Tia nuru akilini –
Na upendo mioyoni – | 9. Ufukuze mashetani –
Na amani tupe hima – |
| 5. Osha machozi yetu
Na kuponya majeraha – | 10. Wape waamini wako –
Paji zako zote saba – |

NJOO ROHO MFARIJI (Andrew Ojiambo)

Tn. Njoo roho mfariji

All: Njoo roho njoo kwetu x2

Tujaze mapaji yako saba

Njoo roho njoo kwetu njoo x2

1. Hekima tushushie akili tujalie, imanni tuzidie njoo kwetu njoo.
2. Tueneze shauri, tuzidishie nguvu, tusifanye ulengevu njoo kwetu njoo.
3. Elimu tueleze, hakika tuongoze ibada tuwashie njoo kwetu njoo.
4. Uchaji tupatie dhambi tuichukie tuonyeshe njia yako njoo kwetu njoo.

PART IX: INAUGURATION OF THE BLESSED SACRAMENT

After the period of silence the celebrant standing prays:

Main Celebrant (Nuncio): Lord, through these gifts increase the vision of your truth in our minds. May we always worship you in your holy temple and rejoice in the presents of all your Saints.
Grant this through Christ our Lord.

R: Amen.

NAKUABUDU YESU

1. Nakuabudu Yesu katika Hostya
U. Mungu kweli na mwanadamu katika Sakramenti

V. Nakwabudu

W. Nakwabudu, fudifudi, ee Mfalme mtukufu wa milele

2. Ee Yesu kwa mapendo unakaa kwetu
U mgeni wetu toka mbinguni, twakuja kuabudu
3. Baraka yako Yesu utupatie
Tukinge na maovu ya leo, tuishi kwa amani
4. Uwabariki pia wapenzi wetu
Uwajalie neema yako, watoe shukrani kuu

Bishop returns to the altar, genuflects, and incenses the Blessed Sacrament.
Bishop receives the humeral veil and blesses the congregation with the Blessed Sacrament

Bishop moves to the tabernacle with mass servers carrying lighted candles.

Bishop places the pyx in the tabernacle, the door of which remains open.

Then incenses the Blessed Sacrament and closes the door of the tabernacle.

Bishop lights the lamp.

The Procession then returns to the Sanctuary.

RITE OF DEDICATION OF A CHURCH

Nuncio and Bishop proceed from the Chapel to the entrance of the Church where the people are gathered. No lights are used.

At this point no incense is used either in the procession or at the Altar.

PART I ENTRANCE INTO THE CHURCH

a) At the entrance of the Church.

Bishop receives miter and pastoral staff.

Words of welcome to the assembly by the Local Bishop.

Words from Architect (in a few words addresses the Bishop and the community, pointing out what the new church expresses in its art and its own special design).

Unveiling of the Paque.

OPENING OF THE DOOR

Contractor hands over the keys and legal documents for possession of the building to the Local Bishop.

Nuncio knocks the door with his staff three times.

Bishop/ Priest In-charge, opens the doors of the Church.

Nuncio invites the people to enter the Church.

ENTRANCE SONG

TWENDE SOTE

*Twende sote nyumbani mwake
Bwana Mungu (aee) twende sote nyumbani mwake aliyetuumba.*

1. Yeye ndiye kinga yetu – Bwana Mungu aee....
Yeye ndiye nguvu yetu – Bwana Mungu aee...
2. Yeye Bwana wa Majeshi –
Ndiye Mungu wa Yakobo –
3. Mtawala wa dunia –
Ni mfalme wa mbinguni –
4. Ndiye Mungu wa wokovu –
Ni hakimu wa dunia
5. Jina lake litukuzwe –
Ndiye Mungu mtakatifu –
6. Yeye apendaye haki –
Ndiye Mungu mwema sana –
7. Yeye Mungu wa rehema –
Mungu wetu wa milele –

NIMEINGIA HAPA MAHALI PATAKATIFU

*Nimeingia (Kwako) hapa mahali patakatifu unipokee (kwako)
unitakaze nipate neema*

1. Nimeingia kwako nimeingia hapa mahali patakatifu.
2. Ee Bwana mwema wewe mfadhili sana nakuja kwako kukutukuza.
3. Nakuabudu pia nakusujudu, nisaidie mimi ni wako.
4. Mimi mkristu pokea sala zangu, Ninakuomba msaada wako.
5. Nihurumie kwani mimi mnyonge Nategemea msaada wako.
6. Unipokee kwako unipokee, unitakase unipe neema.

THANKSGIVING

MOYO WANGU WAMTUKUZA

Moyo wangu wamtukuza Bwana, (Roho) Roho yangu inafurahi x2

1. Kwa kuwa amemwalia, kwa huruma mtumishi wake, hivyo tangu sasa watu wote, wataniita mwenye heri
2. Kwa sababu mwenyezi Mungu, Amenifanyia makuu, jina lake ni takatifu
3. Huruma yake ni kwa wote, wote wale wanaomcha, kizazi hata na kizazi
4. Huyatenda mambo makuu, kwa nguvu za mkono wake, wenye kiburi hutawanya
5. Hushusha wote wenye vyeo, kutoka viti vyao vya enzi, nao wote wanyenyekevu, wote hao huwainua
6. Huwashibisha wenye njaa, na matajiri huwaacha, waende mikono mitupu
7. Hulilinda taifa lake, teule na mtumishi wake, kikumbuka rehema zake
8. Kama alivyo waahidia, babu zetu kawaahidia, Ibrahim na uzao wake.
9. Atukuzwe Baba na mwana, naye Roho mtakatifu, leo, kesho hata milele, kwa shangwe milele Amina

BWANA ALITUTENDEA MAMBO MAKUU

*Bwana alitutendea mambo makuu x2
Tulikuwa tukifurahi furahi x2*

1. Visiwa vyote viimbe kwa furaha,
Bwana ametutendea makuu.
2. Bahari nayo ivume kote kote
Bwana ametutendea mambo makuu.
3. Dunia na vyote viijazavyo kote,
Miti milima icheze kwa furaha.
4. Utukufu na ukuu una yeye
Milele na milele yote. Amina

HIKI NI CHAKULA (SHOMALI)

1. Kuleni mwili wake Bwana mpate uzima kunyweni damu yake Bwana mpate ushindi... x2
Hiki nichakula (chakula) chakula toka mbinguni, sio kama mana ya jangwani wakala wakafa.
2. Anayekula mwili wangu na kuinywa damu hakika anao uzima kutoka mbinguni.
3. Karibuni mezani pake tule pia tunywe chakula kutoka mbinguni uzima tosha.
4. Songea ndugu uionje karamu ya mbingu yashinda karamu za nchi na za wanadamu.
5. Tunakombolewa kwa kifo chake msalabani tunapata taji ya kweli tukifa na Yesu.

BWANA SISTAHILI

Bwana kweli sistahili mimi uingie kwangu

Lakini sema neno moja sema neno moja Bwana x2 sema neno moja Bwana sema neno moja Bwana. Sema neno Bwana na roho yangu itapona x2

1. Mimi mdhahifu, mimi mwenye shida,
Mara naanguka, mara nasimama
2. Leo nina raha, kesho ni huzuni
Ninakasirika, bila ya sababu
3. Ninawaza mema, mengine mabaya
Sina msimamo, unihurumie
4. Mwili wako dawa, yake shida zangu
Bila wewe Bwana, mimi sio kitu.

ROHO YANGU

Roho yangu Yesu inakutamani njoo kwangu Yesu unipe heri

1. Nakupenda kwani wewe mwema, Uniimarisha siku zote.
2. Uje kwangu Yesu nakungoja, Kwani wewe u rafiki mkuu.
3. Maumbo ya mkate na divai, Umo ndani kweli nasadiki.
4. Na uzidi Yesu kuwa name, Unipe uzima wa milele

b) Entrance into the Church

Order of Procession

Cross bearer
Deacon with the Book of the Gospel.
Mass Servers.
Deacons
Main Celebrants
Bishops
Priests
Choir
Religious Sisters
Faithful.

Bishop goes to his chair.

PART II BLESSING AND SPRINKLING OF WATER.

Bishop blesses water with which to sprinkle the people walls and the altar of the new Church by inviting all to pray :

NIMEONA MAJI

Nimeona maji yakitoka hekaluni, upande wa kuume aleluia x2

1. Na watu wote waliofikiwa, Na maji hayo wataokoka,
Nao watasema aleluia.
2. Mshukuruni Mungu kwa maana ni mwema, mshukuruni kwa maana,
Huruma yake ni ya milele.
3. Atukuzwe Baba, pia na Mwana
Atukuzwe Roho Mtakatifu, Kama mwanzo sasa na milele

- Bishop/Priest/Deacon sprinkles with water the congregation and the walls.
- Sprinkling of the altar.
- Bishop returns to the chair and while standing.

KYRIE & GLORY

MISA KARIOBANGI (TB 1-7)

BWANA UTUHURUMIE

V: Utuhurumie

W: Ee Bwana, ee Bwana, ee Bwana

V: ee Bwana (x3), Bwana utuhurumie

V: Utuhurumie

W: Ee Kristu (3)

UTUKUFU

V (Bass) au Padre

Utukufu juu kwa Mungu, utukufu juu mbinguni

W. Na Amani kote duniani kwa wenye mapenzi mema

1. V:(Soprano)

Tunakusifu, tunakuheshimu, tunakuabudu, tunakutukuza, twakushukuru
kwa ajili ya utukufu wako mkuu.

*W: Utukufu juu kwa Mungu, utukufu juu mbinguni, na Amani kote
duniani, kwa wenye mapenzi mema*

2. Ewe Mungu, ndiwe mfalme wa mbinguni,

Baba mwenyezi, ewe Bwana Yesu Kristu, wa pekee mwana wa Baba.

3. Ewe Yesu, mwanakondoo wa Mungu, mwana wa Baba, ewe mwenye kuzion-
doa dhambi zetu tuhurumie.

4. Ewe mwenye kuziondoa za dunia, dhambi za watu, ewe mwenye rehema
nyingi, upokee maombi yetu.

AULAYE MWILI WANGU

*Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu (Asema Bwana)
hukaa ndani yangu nami hukaa ndani yake x2.*

1. Aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu, ana uzima wa milele
2. Njoni enyi wenye njaa, njoni enyi wenye kiu, njoni kwangu niwashibishe
3. Aniaminiye mimi, na kuyashika niyasemayo, nitamfufua siku ya mwisho
4. Mlapo chakula hiki, mnywapo kikombe hiki, mwatangaza kifo cha
Bwana

MWILI WA BWANA YESU

1. Mwili wa Bwana Yesu, chakula cha mbingu ni chakula cha roho, chenye
uzimax2
*(Hima uwe nasi ee Bwana Yesu ukatushibishe chakula bora
(ni chakula cha roho chenye uzima)x2*
2. Yesu alituambia, yeye ni chakula ni chakula cha roho chenye uzima.
Anilaye mimi na kunywa damu anao uzima wa siku zote
(ni chakula cha roho chenye uzima) x2
3. Yesu alituambia, kuwa tumpokee ni chakula cha roho chenye uzima sote
twaamini ni mwili wake, pia twaamini ni damu yake (ni chakula cha roho
chenye uzima) x2
4. Hii ndiyo karamu aliyotuachia, ni chakula cha roho chenye uzima. Ee
Bwana mwokozi tunakuomba, kwa chakula hiki tuimarike (ni chakula cha
roho chenye uzima) x2

EKARISTIA

*Ekaristia ni chakula, chakula cha uzima wa milele, ee mkate
wa mbinguni shibisha roho zetu x2*

1. Yesu mwokozi kashuka chini kwetu tukampokee.
2. Maumbo haya ni mwili wake Yesu twakiri sote.
3. Yesu mpenzi pokea moyo wanu name ni wako.
4. Ninakupenda kuliko nafsi yangu mwokozi wangu.

EUCHARISTIC PRAYER III (SEE ANNEX)**ANAYEKULA MWILI WAKO (TB – 8-23)**

1. Anayekula mwili wako na anywaye damu yako anaishi ndani yako, ye hatakufa milele.

Wote: Yesu wangu nakuomba, nishibishe na mwilio, nayo damu yako ninywe japo sistahili mimi.

2. Ndani yangu mwokozi yumo, kwa mwili na damu yake, ni rafiki yangu kweli, nami sitamwacha kamwe.
3. Alikuwa kutuokoa, tuliokuwa dhambini, kwa kifo chake msalabani, naye katupa uzima.
4. Yesu wangu, unibariki, nifundishe njia zako, nipe moyo wa shukrani, nitembe nawe leo.

TWENDENI KWA KARAMU (TB 8-8)

1. V: Twendeni kwa karamu ya Bwana tumeitwa
W: Twendeni, twende kumpokea.
V: Ni mwaliko wa Bwana
W: Tukale mkate wa uzima
2. Tujitakase mbele ya kwenda kwa karamu hii
Twende watakatifu
3. Karibu kwangu Yesu, ukae kwangu daima,
Nifunze njia zako
4. Na kwa uwezo wako Imani yangu nakiri,
Ndiwe Mungu mwokozi.
5. Usituache basi pamoja nasi ukae,
Kwa kuwa kumekuchwa.
6. Na tufurahi mwisho pamwe na Baba milele,
Kwa umoja na Roho.

5. Uketiye kuume kwake Mungu Baba, tuhurumie, kwa kuwa ndiwe uliye peke yako mtakatifu.
6. Pekee yako ni wewe Bwana, peke yako Bwana mkuu, pekee yako ni mkombozi, peke yako Yesu Kristu.
7. Naye Roho mtakatifu, katika tukufu wake, Mungu moja anayeishi na kutawala milele yote.

PART III LITURGY OF THE WORD**HYMN FOR PROCESSION OF THE WORD.****INJILI****INASONGA MBELE INJILI**

Inasonga mbele injili – inasonga, inasonga mbele injili inasonga mbele x2.

1. Injili ya amani –
Injili ya upendo –
2. Injili kwa wababa –
Injili kwa wamama-
3. Injili kwa vijana –
Injili kwa watoto

NIPE NENO LA MUNGU

*Nipe Neno la Mungu Neno la Mungu.
Nipe Neno safi Neno safi.*

1. Nimekuja Kusikia Neno la Mungu kusikia
2. Yesu ataniuliza ulifanya nini duniani
3. Yesu atawachukuwa watu wake kuenda mbinguni.

Bishop standing with the Mitre receives the Lectionary and shows to the people while saying

May the Word of God always be heard in this place, as it unfolds the mystery of Christ before you and achieves your salvation within the church.

SOMO LA KWANZA

Nehemia 8:1-10

Somo katika kitabu cha Nehemia

Siku zile:

Naye Ezra, kuhani, aliileta Torati mbele ya mkutano uliojaa wanawake na wanaume na wengine wote waliofahamu, katika siku ya kwanza ya mwezi wa saba. Akiwa amesimama upande mmoja wa mahali pa wazi akikabili Lango la Maji, Ezra alisoma kutoka humo kitabuni tokea alfajiri hadi aduhuri, mbele ya wanaume na wanawake, na watoto waliowakubwa kuelewa; na watu wote walisikiliza kwa makini, yote yaliyosomwa kutoka katika kitabu cha Torati. Naye Ezra, kuhani, akasimama juu ya jukwaa la miti iliyojengwa kwa kusudi hilo. Ezra alifungua kitabu mbele ya macho ya watu wote, maana alisimama mahali pa juu zaidi kuliko watu wote. Watu hao wakasimama wima mara tu alipokifunua kitabu.

Ezra akamtukuza Bwana, Mungu mkuu, na watu wote huku wakiwa wameinua mikono yao juu, wakitikia, “Amina, amina!” Halafu wakainama chini nakumsujudu Bwana kifudufudi. Naye Ezra akasoma kutoka katika kitabu cha Sheria ya Mungu, akiitafsiri ili watu waweze kuelewa kilichotafsiriwa. Halafu Nehemia, yaani gavana, na Ezra, kuhani-mwandishi, na Walawi waliokuwa wakifahamika na watu waliwaambia watu wote, “Leo ni siku takatifu kwa Bwana Mungu wetu. Hivyo msiwe na huzuni na wala msilie” maana watu wote walikuwa wanalia walipoyasikia maneno ya sheria.

Akaendelea, “Nendeni mkale chakula bora na vinywaji vitamu, na kutenga sehemu kwa wale watu ambao hawakutayarisha chochote; kwani leo ni siku takatifu kwa Bwana wetu. Msisikitike leo, kwa kuwa kufurahi katika Bwana ndio nguvu yenu!”

Neno la Bwana.

PART VIII LITURGY OF THE EUCHARIST

When the preparation of the Altar is ready

Bishop goes to the Altar, removes the Mitre and kisses the Altar.

PRAYER OVER THE GIFTS

Main Celebrant (Nuncio): Lord, accept the gifts of a rejoicing Church may your people who are gathered in this sacred place, arrive at eternal salvation through the mysteries in which they share. Grant this through Christ our Lord.

R: Amen.

Preface

Sactus.....

V. (Bass) Mtakatifu

W. Mtakatifu, Mtakatifu, Bwana Mungu

V. (Bass) Wa majeshi

W. Mbingu na dunia zimejaa ‘tukufu wako

V. (Tenor) Hosana W. Hosana juu mbinguni

V. (Tenor) Hosana W. Hosana juu mbinguni

V. (Bass) Mbarikiwa

W. Anayekuja kwa jina lake Bwana Mungu

V. (Tenor) Hosana W. Hosana juu mbinguni

V. (Tenor) Hosana W. Hosana juu mbinguni

Great Amen

AGNUS DEI

V. (Sop) Ee Mwanakondoo

W. Uondoaye dhambi za dunia, utuhurumie

V. (Tenor) Ee Mwanakondoo

W. Uondoaye dhambi za dunia, utujalie amani

UTUKUZWE, EWE BABA (TB)

1. V. Utukuzwe, ewe Baba, Mungu, utukuzwe –
W. Aleluya
V. Kwani Yesu mfufuka ametualika –
Kiitikio
V: Utukuzwe
W: Utukuzwe
V: Baba, Mwumba ulimwengu x2
W: Aleluya
2. Tumepokea mkate, mazao ya mashamba - Aleluya
Ndio alama kwetu ya wema wako mkuu - Aleluya
3. Ni tunda la bidii ya mkono na ya moyo - Aleluya
Jalia uwe kwetu chakula cha uzima - Aleluya
4. Zawadi ya divai kutoka mizabibu - Aleluya
Ndiyo alama kwetu ya wema wako mkuu - Aleluya
5. Sifa kwako, ee Mungu, kwa kuotesha mkate - Aleluya
Shukrani kwako Baba, kwa kutulisha sisi - Aleluya
6. Utukuzwe, ee Mungu, uliyetuchagua - Aleluya
Tuwe taifa lako na kukutumikia - Aleluya

ZABURI YA KUITIKIZANA

ZABURI 19:8,9,10,15(K. taz. Yohane 6:63c)

K. Maneno yako, ee Bwana, ni roho, tena ni uzima

Sheria ya Bwana ni kamilifu,
ya utuliza moyo.
Maagizo ya Bwana ni imara, yamletea mjinga hekima. **K**

Amri za Bwana ni za haki,
zaufurahisha moyo,
agizo la Bwana ni safi, layatia macho mwangaza. **K**

Uchaji wa Bwana ni safi,
hudumu hata milele,
Hukumu za Bwana ni kweli, zote ni za haki kamili. **K**

Maneno ya kinywa changu
yakupenze wewe,
nayo mawazo ya moyo wangu,
yaliyo mbele yako, ee Bwana,
Mwamba wangu na Mkombozi wangu. **K**

Ufunuo 21:1-5

SOMO LA PILI**Somo katika kitabu cha Ufunuo wa Mtakatifu Yohane**

Mimi, Yohane, niliona mbingu mpya na nchi mpya kwani mbingu ya kwanza na ulimwengu wa kwanza vilikuwa vimepita, na bahari haipo tena.

Nikauona mji mtakatifu, Yerusalemu mpya, ukishuka kutoka mbinguni kwa Mungu. Umetayarishwa kama bibi harusi aliyejipamba kwa ajili ya mume wake. Nikasikia sauti kubwa kutoka kiti cha enzi ikisema, “Tazama hema ya Mungu kati ya wanadamu. Naye atakaa kwao, nao watakuwa taifa lake na Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao.

Atafuta kila chozi katika macho yao. Hakutakuwa tena wala mauti, wala sikitiko, wala kilio, wala maumivu kwa kuwa mambo ya kwanza yatakuwa yamepita.” Yeye aliyeketi katika kiti cha enzi akasema, “Tazama, nafanya yote upya.”

Neno la Bwana.

INJILI

Mathayo 16:13 - 19

“Wewe ndiwe Petro, na nitakupa funguo za ufalme wa Mbinguni.”

Somo la injili mtakatifu ilivyoandikwa na Mathayo

Wakati ule: Yesu aliingia sehemu ya kaisaria filipi. Akawauliza wafuasi wake, “Watu wanasema mwana wa mtu ni nani?” wakasema, “Wengine Yohane mbadisaji, wengine Eliya, tena wengine Yeremiah au mmojawapo wa manabii.” Akawaambia, “Na ninyi mnasema mimi ni nani?” Simoni Petro akajibu, “Wewe ndiwe Kristo, mwana wa Mungu mzima.” Yesu akamjibu, “Una heri wewe Simoni mwana wa Yona, kwa maana si mwili na damu vilivyokufunulia hayo, isipokuwa Baba yangu aliye Mbinguni. Nami nakuambia, wewe ndiwe Petro, na juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu, na milango ya Jehanamu haitalishinda. Na wewe nitakupa funguo za ufalme wa Mbinguni. Lolote utakalofunga duniani, litafungwa Mbinguni pia; na lolote utakalofungua duniani, litafunguliwa Mbinguni pia.”

Injili ya Bwana

MUNGU BABA POKEA (TB 5-7)

1. Mungu Baba pokea sadaka yetu leo,
Twakutoleayo kwa jina la mwanao,
Ya Abeli na Ibrahim ilikupendeza,
Yetu Baba ipendeze, upokee tu
K: Upokee W: Sadaka yetu
K: Ndilo fumbo W: La kukupendeza
K: La Baba W: Na mwana, na Roho mtakatifu x2
2. Njoni wote tutoe sadaka yetu leo
Kwa sifa na utukufu wake mwenyezi,
Mkate huu na divai viwe mwili wake
Kwa heshima kuu sadaka tumtolee.
3. Ee Mwenyezi tupokee tuwe mali yako
Twakusihhi kwa shukrani kuu tupokee
Tunakutolea nguvu, kazi na mavuno
Kwa huruma yako dhambi tuondolee.
4. Kama mwanzo Mungu Baba nasi asifiwe na mwanaye ndiye
aliyetukomboa,
Roho Mtakatifu ndiye wetu mfariji
Tatu mtakatifu Mungu mmoja twakiri

EE BWANA TWAKUOMBA

Ee Bwana twakuomba upokee vipaji vyetu x2. Hivyo vyote ni mali yako tumepata kwa wema wako pokea x2.

1. Mkate divai twakuomba, twakuomba Baba upokee.
2. Mawazo yetu pia matendo, twakuomba Baba upokee.
3. Twakutolea na nyoyo zetu, kwa upendo Baba upokee.
4. Fedha na mali tulizo nazo, twakuomba Baba upokee.

BWANA UPOKEE ZAWADI (TB 5-8)**Wote: Bwana, upokee (x2), Zawadi twaleta**

- | | |
|----------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------------|-------------------------------------------------------------------------------------------------------------|
| 1. Mkate na divai – Zawadi twaleta
Mazao ya mashamba – Zawadi twaleta
Na pia nafsi zetu - Zawadi twaleta
Vyote tulivyo navyo - Zawadi twaleta
Furaha na uchungu - Zawadi twaleta | 3. Kwako Baba muumba –
Kwa njia ya mwolozzi –
Katika mfariji –
Ipate kugeuzwa –
Iweze kutufaa – |
| 2. Na kiini cha ngano –
Na tunda la mzabibu –
Fedha za mifukoni –
Nafaka upokee –
Twakutolea vyote – | 4. Pokea, twakuomba –
Ingawa ni kidogo –
Twatolea kwa moyo –
Baba, usikatae –
Vipaji vya wana |

EE BWANA, VYOTE MALI YAKO (TB 5-9)**Wote: Ee Bwana, vyote mali yako,
(Bwana) twakupa vyote mali yako.**

1. Pokea mkate na divai – Bwana twakupa vyote mali yako.
2. Mazao ya mashamba yetu – Bwana twakupa vyote mali yako
3. Pokea nazo nia zetu – Bwana twakupa vyote mali yako
4. Pokea nazo nyoyo zetu – Bwana twakupa vyote mali yako
5. Na fedha za mifuko yetu – Bwana twakupa vyote mali yako
6. Na kazi za mikono yetu – Bwana twakupa vyote mali yako
7. Furaha na uchungu wetu – Bwana twakupa vyote mali yako

KANUNI YA IMANI YA NICENE

Nasadiki kwa Mungu mmoja Baba mwenyezi,
Muumba wa mbingu na dunia na vitu vyote vinavyoonekana
na visivyooonekana.

Nasadiki kwa Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwanae pekee wa Mungu,
aliyezaliwa kwa Baba tangu milele yote.
Mungu aliyetoka kwa Mungu, mwanga kwa mwanga,
Mungu kweli kwa Mungu kweli, aliyezaliwa, bila kuumbwa, mwenye
umungu mmoja na Baba: ambaye vitu vyote vimeumbwa naye.
Alishuka kutoka mbinguni, kwa ajili yetu sisi wanadamu,
na kwa ajili ya wokovu wetu, akatwaa mwili kwa uwezo wa Roho Mtakatifu,
kwake yeye Bikira Maria, akawa mwanadamu.
Akasulubiwa kwa ajili yetu sisi, kwa mamlaka ya Ponsyo Pilato; akateswa,
akafa, akazikwa, siku ya tatu akafufuka,
kadiri ya Maandiko, akapaa mbinguni, amekaa kuume kwa Baba.
Atakuja tena kwa utukufu, kuwahukumu wazima na wafu,
nao ufalme wake hautakuwa na mwisho.

Nasadiki kwa Roho Mtakatifu, Bwana mleta uzima:
atokaye kwa Baba na Mwana.
Anayeabudiwa na kutukuzwa, pamoja na Baba na Mwana:
aliyenena kwa vinywa vya manabii.

Nasadiki kwa Kanisa moja, takatifu, katoliki, la Mitume.
Naungama ubatizo mmoja kwa maondoleo ya dhambi.
Nangojea na ufufuko wa wafu,
na uzima wa milele ijayo.

Amina.

KANUNI YA IMANI YA MITUME

Nasadiki kwa Mungu, Baba Mwenyezi, mwumba mbingu na dunia.
Na kwa Yesu Kristu, Mwanaye wa pekee, Bwana wetu; aliyetungwa kwa

Roho Mtakatifu,
akazaliwa na Bikira Maria,
akateswa kwa mamlaka ya Ponsyo Pilato,
akasulubiwa, akafa, akazikwa, akashukia kuzimu;
siku ya tatu akafufuka katika wafu;
akapaa mbinguni; amekaa kuume kwa Mungu Baba Mwenyezi;
toka huko atakuja kuwahukumu wazima na wafu.

Nasadiki kwa Roho Mtakatifu,
Kanisa takatifu katoliki,
ushirika wa Watakatifu,
maondoleo ya dhambi,
ufufuko wa miili, uzima wa milele.

Amina.

TUTOE SADAKA

BASS: Tutoe sadaka

ALL: Kwa Mungu Baba aliyemba ulimwengu mzima. x2
Tukumbuke kwamba ndiye aliyetupa uzima tutoe sadaka x2.

1. Tutoe kwa moyo mwema tukampe Bwana
Na kwa ukarimu mwema tutoe kwa moyo.
2. Na hii siku ya leo tukampe Bwana, ndugu usifiche nenda ukamoe
Bwana.
3. Nazo fedha zako nenda ukampe Bwana,
Ndugu usisite nenda ukampe Bwana.

BABA TUNALETA VIPAJI

1. a. Baba tunaleta vipaji twakuomba sana Pokea
– Baba tunaleta twakuomba sana pokea.
b. Twaja kushukuru kwa yote ulotujalia wanao
– Baba tunaleta twakuomba sana pokea.
***Baba tunasema asante asante (kutupa uzima) asante asante
(kwa kutombo) asante asante (kutuweka huru) asante
asante***
2. a. Mkate na divai twaleta twakuomba sana pokea.
b. Ndiyo kazi yetu wanao twakuomba sana pokea.
3. a. Mazao ya mashamba twaleta twakuomba sana pokea.
b. Hata ni kidogo twaleta twakuomba sana pokea.
4. a. Nazo fedha zetu twaleta twakuomba sana pokea.
b. Utupe Baraka twaleta twakuomba sana pokea.

SADAKA YANGU

Sadaka yangu kwako Ee Mungu

Ni moyo mnyofu na uliopondeka

Tazama wapendezwa na kweli ya moyo

nawe wanijalia hekima kwa siri,

Nioshe kabisa na uovu wangu na

kinywa changu kitanena sifa zako.....

1. Maana wewe Bwana hupendezwa na dha-bihu za kuteketezwa ama sivyo mimi ningali kutolea....
2. Wapendezwa na dhabihu za haki kuto-ka- kwa moyo mnyofu zitolewazo juu ya madhabihu yako....
3. Ee Mungu wa wokovu wangu unipe moyo radhi wa utii usinindolee roho wako mtakatifu....

ALFAJIRI YA KUPENDEZA

TN: Alfariji ya kupendeza ni siku njema siku yenye Baraka ...

ALL: Jua limekwisha chomoza laamsha wote waliolala, ndege nao wanalia kumshukuru muumba (njooni) (Njooni Baba mama na watoto njooni wote mbele za Bwana tumtolee shukrani zetu kwa kutoa sadaka x2)

1. Ndege wanamshukuru kwa sauti za kupendeza, na sisi tumshukuru kwa zawadi alizotupa (njooni).
2. Wanyama pia na mimea, vyote vimeumbwa na Mungu, vitu vya duniani vyapaswa kumshukuru Mungu (njooni).
3. Kaiumba dunia hii kaweka giza pia mwanga, mchana tufanyeni kazi usiku na tupumzike (njooni)

PART IV PRAYER OF DEDICATION AND THE ANOINTING

Prayers of the faithful are replaced by the Litany of the Saints. v Bishop without Miter and Staff invites all to pray:

Main Celebrant (Nuncio): Let us ask the saints to support our prayers to God the Father Almighty, who has made the hearts of his people faithful temples of His Spirit.

On Sundays and Easter Season all stand/ other days all kneel.

LITANIA YA WATAKATIFU

Bwana, utuhurumie
Kristu, utuhurumie
Bwana, utuhurumie

Bwana, utuhurumie
Kristu, utuhurumie
Bwana, utuhurumie

Maria Mtakatifu, Mama wa Mungu
Mtakatifu Mikaeli
Watakatifu Malaika wa Mungu
Mtakatifu Yosefu
Mtakatifu Yohana Mbatizaji
Mtakatifu Petro na Mtakatifu Paulo
Mtakatifu Andrea
Mtakatifu Yohani

Utuumbee
Utuumbee
Mtuombee
Utuumbee
Utuumbee
Mtuombee
Utuumbee
Utuumbee

Mtakatifu Basili
 Mtakatifu Martino
 Mtakatifu Benedikto
 Mtakatifu Fransisko na Mtakatifu Dominiko
 Mtakatifu Fransisko Xaveri
 Mtakatifu Yohane Maria Viane
 Mtakatifu Teresia wa Avila
 Mtakatifu Katarina wa Siena
 Watakatifu Mashahidi wa Uganda
 Mtakatifu Bakhita
 Mtakatifu Yohane wa ishirini na tatu
 Mtakatifu Yohane Paulo wa Pili
 Watakatifu wote wa Mungu
 Utuhurumie
 Katika mauti ya milele
 Kwa kujifanya mwanadamu
 Kwa kufa na kufufuka kwako
 Kwa kumpeleka Roho Mtakatifu
 Sisi Wakosefu

Utuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Mtuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Mtuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Utuombee
 Mtuombee
 Utuokoe, Bwana
 Utuokoe, Bwana
 Utuokoe, Bwana
 Utuokoe, Bwana
 Utuokoe, Bwana
 Twakuomba utusikie

Main Celebrant (Nuncio) sings while blessing the Congregation

Upende kulisimamia na kulilinda kanisa lako takatifu,
**Twakuomba utusikie**
 Upende kumlinda Baba Mtakatifu na wote wenye daraja katika dini takatifu,
**Twakuomba utusikie**
 Upende kuwajalia mataifa yote amani na mapatano ya kweli,
**Twakuomba utusikie**
 Upende kutudhibitisha sisi na kutudumisha katika utumishi wako mtakatifu,
**Twakuomba utusikie**
 Upende kilitakasa kanisa hili,
**Twakuomba utusikie**

OFFERTORY

LETENI SADAKA

Leteni sadaka kamili ghalani x2 (ili) chakula kiwemo katika nyumba ya-ngu asema bwana (wamajeshi) bwana wa majeshi x2.

1. Mkanjaribu kwa njia hii asema Bwana.
 Nitafungua milango ya mbinguasema Bwana.
 Nakumwagia Baraka tele....asema Bwana.
2. Mimi ndimi mgawa wa vipaji.
 Nitawaongezea maarifa....
 Na kuyashinda magumu yote....
3. Mtakachokiomba nitawapa....
 Nitawapa vyeo na mali nyingi
 Na kuuondoa umaskini
4. Nitawalinda na kuwastawisha
 Nanyi mtazaa matunda bora.....
 Yatakayodumu milele yote

SIKU MOJA ZAKAYO

Nimemdhulumu mtu nitamrudishia mara nne, yeyote niliyemdhulumu nitarudisha kwake mara nne x2

1. Zakayo akasema yote nimekubali kugawanya mali yangu kwao masikini, na mimi leo hii nitoaposadaka nibariki nigawie na wengi.
2. Mali nilizo nazo zote zatoka kwako pokea shukrani, japo ni kidogo najitoea mwenyewe na matatizo yangu nitoayo ndogo baba ibariki.
3. Mazao ya shambani nатоa nikijua shamba ulinipa nikutumikie, fedha nilizonazo na mshahara wangu nguvu zako Mungu ulinjalia.
4. Jana hata na leo ni majaliwa yako nibariki kesho nayo niione, sio kwa nguvu zangu bali kwa nguvu zako uliyeiumba dunia na sisi.

SALA YANGU**Sala yangu na ipae mbele yako ...kama moshi wa ubani x2**

1. Ee Bwana upokee sadaka yetu tunayokutolea kama shukrani yetu Ee Bwana pokea
2. Ee Bwan upokee dhabihu zetu tunazokutolea kutoka mashambani Ee Bwana pokea.
3. Ee Bwana upokee pia nia zetu tunazokutolea kwa moyo wetu wote Ee Bwana pokea.

PART VII LIGHTING OF THE ALTAR AND THE CHURCH**Bishop lights the candles saying:**

Main Celebrant (Nuncio): Light of Christ, shine forth in the Church and bring all nations to the fullness of truth.

Bishop/Priest/Deacon/ lights the rest of the 12 candles for the walls. v Other candles are lighted for the altar.

CHOIR LEADS A HYMN**MWANGA WA KRISTU**

1. Mwanga wa Kristu utuangaze x2
2. Kristu mfufuka ...
3. Giza ondoa
4. Kwako tufike ...
5. Tukutambue
6. Tukufuate
7. Ewe Mtukufu...
8. Dhambi tuoshe

Upende kulitakasa kanisa hili na kulitia wakfu kwa ibada takatifu,
.....*Twakuomba utusikie*

Choir continues

Yesu Mwana wa Mungu aliye hai, **Twakuomba utusikie.**
Kristu, utusikie, **Kristu utusikie.**
Kristu, utusikie, **Kristu utusikie**

After the litany the Bishop without Mitre stands with hands extended and says:

Main Celebrant (Nuncio): Lord, may the prayers of the Blessed Virgin Mary and all the Saints, make our prayers acceptable to you.

May this building, which we dedicate to your name, be a house of salvation and grace, where Christians gathered in fellowship may worship you in spirit and truth and grow together in love.

Grant this through Christ our Lord.

R: Amen.

DEPOSITING OF THE RELICS

Bishop receives the Mitre
Bishop approaches the altar to place the relics

PRAYER OF DEDICATION.

**PART V:
ANOINTING OF THE ALTAR AND THE WALLS OF THE CHURCH**

Bishop standing before the Altar says:

Main Celebrant (Nuncio): We anoint this altar and this building. May God in his power make them holy, visible signs of the mystery of Christ and his Church.

He removes the chasuble and puts on the linen gremial.

Bishop pours chrism on the middle of the altar and on each of its corners and anoints the entire table of the Altar with Chrism.

The walls of the church are also anointed with the assistance of Bishops/Priests

HYMN FOR ANOINTING

INUKENI MALANGO

Inukeni enyi malangoEnyi malango ya milele mfalme wa utukufu apate kuingia x2

1. Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya Bwana...dunia nao watu wote wakaa ndani yake....
2. Maana ameweka misingi juu ya bahari na juu ya mito ya maji aliithibitisha...
3. Ni nani atakayepanda mlima wa Bwana....
Nani atakayesimama patakatifu pake....
4. Mtu mwenye mikono safi na mwoyo mweupe asiyeinua nafsi yake kwa ubatili....
5. Hiki ndicho kizazi chao wamtafutao...Wakutafutao Ee Mungu Ee Mungu wa Yakobo...
6. Inueni na vichwa vyenu Enyi malango ...mfalme ni wa utukufu apate kuingia....

MASKANI ZAKO

Maskani zako zapendeza kama nini....Ee Bwana Ee Bwana wa Majeshi x2

1. Nafsi yangu inazionea shauku nyua za Bwana nyua za Bwana....
2. Moyo wangu na mwili wangu vinamlilia Mungu wangu....
3. Shomoro naye ameona nyumba mbayuwayu amejipatia kiota..
4. Alipoweka makinda yake kwenye madhabahu yako Ee Bwana..
5. Heri wakao nyumbani mwako wanakuhimidi daima...
6. Heri ambaye nguvu zake zatoka kwako sayuni zimo moyoni mwake

v After the anointing of the altar Bishop returns to his chair, washes hands and puts on the chasuble.

PART VI INCENSATION OF THE ALTAR AND THE CHURCH

The celebrant puts incense into the pot placed on the Altar while saying:

Main Celebrant (Nuncio): Lord may our prayer ascend as incense in your sight. As this building is filled with fragrance so may your Church fill the word with the fragrance of Christ.

The Bishop puts incense in the censer and incenses the Altar.

Then the Bishop returns to the chair and is incensed by the deacon/priests and he sits.

Ministers move through the Church incensing people and walls while the altar is being vested/covered with altar clothes.

Candles and flowers' pot are put on the Altar and the altar cross.

Choir sings a suitable hymn.